



**UWASILISHAJI WA NIA YA ZABUNI: USAMBAZAJI WA SAMANI ZA OFISINI KWA MKANDARASI MKUU WA USAFIRISHAJI KATIKA MRADI WA EACOP KUMB NA. EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 05 EOI 0028**



E.A.L.S Limited Tanzania kama Mkandarasi Mkuu wa Usafirishaji wa Mradi wa EACOP, inakaribisha mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuwasilisha nia ya kuomba zabuni ya usambazaji wa samani za ofisini katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la chini linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda, hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati ya hizo kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania

**MAELEZO MAFUPI YA AINA YA HUDUMA ZINAZOHITAJIKA**

Usambazaji, ufikishaji na upangiliaji wa madawati yenye viwango stahiki, makabati ya kuhifadhia nyaraka, viti vya ofisini na makabati ya vyumba vidogo.

**SIFA BAINIFU:** Kampuni zitakazowasilisha nia zinaalikwa kuwasilisha maombi yao na:

- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha uthibitisho wa mlipaji kodi cha mwaka wa karibuni.
- Uthibitisho wa usajili/maombi katika Kanzidata ya Watoto Huduma na Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia linahitajika. (INASISITIZWA).
- Uzingatiaji wa Kanuni za Petroli (Local Content), 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Kizawa nchini Tanzania.
- Uwasilishaji wa Ritani za kodi pamoja na risiti za malipo.
- Nakala ya kitambulisho cha Serikali kwa wadau
- Sera za Kampuni na Taratibu zake i.e. Afya, Usalama na Mazingira, Udhhibiti Utakatishaji fedha, Haki za Binadamu nk.
- Cheti cha usajili kutoka BRELA.
- Mkataba na Katiba ya Kampuni.
- Cheti cha TIN; Leseni na vibali vyote sahihi vya biashara.
- Taarifa za Fedha zilizokaguliwa hivi karibuni.

**Ili kupata maelezo ya kina kuhusu uwasilishaji wa nia hapo juu,** Kampuni ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kuwasilisha nia zao kwa kutuma pamoja na nyaraka ambatanishi zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **TZ009-info.supplier@eals.co.tz** (ukubwa wa mwisho wa utumaji barua pepe 20Mb) ifikapo au kabla ya **9: 00 Alasiri** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **06.09.2023**. kichwa cha barua pepe lazima kiwe kama ifuatavyo: **EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 05 EOI 0028**.

Kumbuka: E.A.L.S Limited itakagua na kutathmini hati zinazotolewa na kampuni zilizowasilisha nia ili kupata orodha ya kampuni zilizokidhi vigezo mapema. Kampuni zilizokidhi vigezo pekee ndizo zitapokea, kulingana na kutiwa saini kwa makubaliano ya siri (NDA), muito wa kuwasilisha zabuni ili kuendeleza mwito wa mchakato wa zabuni. Maombi yote yanapaswa kuwasilishwa kwa Lugha ya Kiingereza.

**E.A.L.S Limited inahifadhi haki ya kutozingatia makampuni ambayo yanawasilisha ripoti ambayo hajakamilika.**